*Wekeza na jenga maisha na SACCOS*

# LESA SACCOS LTD

## REG. No DSR 1299

# SERA YA MENEJIMENTI YA UKWASI, MALI NA DHIMA

WEKA AKIBA MARA KWA MARA, KOPA KWA BUSARA LIPA KWA WAKATI, WEKEZA KWA MAENDELEO YAKO.

TOLEO LA I-2020

## UIDHINISHAJI WA SERA YA MENEJIMENTI YA UKWASI,MALI NA DHIMA

| **Tarehe ya Kupitishwa na Kikao Cha Bodi** | | **Kikao Cha Bodi cha Tarehe 17 Julai 2020** |
|---|---|---|
| **Mpya**<br><br>**Imehuishwa** | ☐<br><br>☐ | **Toleo la: I<br>Mwaka 2020** |

**Imetiwa Saini kwa Niaba ya Wanachama na;**

| S/N | Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EVA .J.BOSCO | Mwenyekiti wa bodi | 23/11/2020 | |
| 2 | GWAMAKA JAPHARI | M/Mwenyekiti bodi | 23/11/2020 | |
| 3 | SEMALY KISAMO | Mjumbe wa bodi | 23/11/2020 | |
| 4 | SHAFII MMILE | Mjumbe wa bodi | 23/11/2020 | |
| 5 | NAOMI SERBANTEZ | Mjumbe wa bodi | | |

**Imetiwa Saini kwa Niaba ya Watendaji na:**

| Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|
| DEONATUS KIHEKA | Meneja | 28/09/2020 | |

**Kwa Matumizi ya Mrajis:**

Maoni ya Mrajis:

| Jina | Wadhifa | Tarehe | Sahihi |
|---|---|---|---|
| | | | |

*Muhuri*

## YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA**......3

**1.0 UTANGULIZI**......3

**1.2 MADHUMUNI NA MANUFAA YA SERA**......4

**SEHEMU YA PILI**......6

**2.0 MENEJIMENTI YA UKWASI, MALI NA DHIMA KATIKA CHAMA**......6

2.1 Watu wanaowajibika na usimamizi wa Ukwasi, Mali na Dhima za Chama......6

2.2 Viwianishi vinavyotumika kupima Ukwasi, Mali na Dhima......7

2.3 Njia zitakazotumika kusimamia Ukwasi, Mali na Dhima za Chama......8

2.4 Kiwango cha juu na chini cha fedha taslimu......10

2.5 Kiwango cha juu cha fedha taslimu kwenye kasiki......10

2.6 Utaratibu wa utoaji wa taarifa ya hali ya ukwasi......10

2.7 Utaratibu wa mara kwa mara wa kuchambua Ukwasi, Mali na Dhima......11

**SEHEMU YA TATU**......11

**3.0 MAHITAJI YA UKWASI**......11

**SEHEMU YA NNE**......12

**4.0 UKOPAJI KUTOKA NJE**......12

**SEHEMU YA TANO**......13

**5.0 MAJUKUMU YA BODI YA CHAMA**......13

**SEHEMU YA SITA**......14

**6.0 MPANGO WA DHARURA WA UKWASISHAJI**......14

6.1 Malengo ya mpango wa dharura wa ukwasishaji......14

**HITIMISHO**......Error! Bookmark not defined.

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

LESA SACCOS LTD ilianzishwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na.20 ya mwaka 2003.Kwa malengo ya kupokea akiba na kutoa Mikopo yenye masharti nafuu kwa wamanachama wake. Mkutano mkuu wa wanachama ndicho chombo cha juu chenye mamlaka katika shughuli zote za chama na kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinatambua kuwa bodi ya chama ndio chombo pekee cha kuongoza chama kwa kuzingatia ukasimishwaji wa madaraka hayo kupitia mkutano mkuu wa wanachama.

Kifungu Na.52 cha Sheria ya Vyama Vya Ushirika kinaenda mbali zaidi na kutoa nafasi kwa bodi kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia chama na miongoni mwa miongozo iliyotajwa ni pamoja na sera ya menejimenti ya ukwasi,mali na dhima.

Chama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) huanzishwa ili kuwawezesha wanachama wake kupata huduma za kifedha kwa gharama nafuu na kwa ukaribu zaidi katika mazingira yaliyo rafiki zaidi. Wanachama wanaweka fedha zao wakiwa na uhakika wa kupata huduma mara wanapohitaji. Huduma zinazotolewa na chama ni pamoja na kununua hisa za uanachama, kuweka akiba na kutoa mikopo kwa wanachama kulingana na Sera za Mikopo za chama. Ili chama kiweze kutoa huduma hizo kinatakiwa kuwa na fedha za kutosha za kukiwezesha chama kulipia gharama mbalimbali kama vile malipo ya mishahara ya watendaji, ada za kisheria na gharama nyingine za uendeshaji.

Katika kuwezesha LESA SACCOS LTD kutimiza wajibu huu, Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018 na Kanuni za huduma ndogo za fedha (SACCOS) za mwaka 2019 inazitaka SACCOS kuwa na Sera ya Usimamizi wa Ukwasi, Mali na Dhima. Mantiki ya kuwa na sera hii ni kuiwezesha SACCOS kujenga uwezo wa kutoa huduma kwa wanachama wake bila kusababisha usumbufu kwa mwanachama husika, pamoja na kujenga uwezo wa kulipia gharama mbalimbali za uendeshaji kwa wakati.

Kupitia sera ya ukwasi, LESA SACCOS LTD inaweka utaratibu wa kutambua mahitaji ya fedha ya muda mfupi na muda mrefu, kupanga mtiririko wa fedha utakaoendana na mahitaji yake, kufanya tathmini ya mara kwa mara ya mfumo wa ukwasishaji na kuwa na mpango mbadala wa dharura wa kupata fedha kuziba pengo la upungufu wa ukwasi ndani ya SACCOS.

Sera hii itatumika sanjari na sera nyingine za LESA SACCOS LTD hasa Sera ya Akiba na Mikopo na ukusanyaji wa madeni chechefu pamoja na Kanuni za Fedha na Uhasibu.

Kutokana na umuhimu wa Sera hii katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa wanachama wa LESA SACCOS LTD, viongozi na watendaji wa LESA SACCOS LTD wanao wajibu wa kuitekeleza sera hii.

## 1.2 MADHUMUNI NA MANUFAA YA SERA

Madhumuni ya Sera ya Menejimenti ya Ukwasi, Mali na Dhima ni kukiwezesha chama kuwa na mfumo thabiti wa kusimamia mali na dhima za chama wakati wote ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua zinazostahili kwa wakati ili kukabiliana na mahitaji ya ukwasi yanayojitokeza.

Sera hii inakusudia kuhakikisha kuwa chama hakipati shida katika kutoa huduma kutokana na ukosefu wa ukwasi na pia kuhakikisha kuwa chama hakiwi na ukwasi zaidi. Kushindwa kwa chama kutimiza wajibu wake kwa sababu ya ukosefu wa ukwasi wa kutosha, kutapelekea wanachama kupunguza imani na chama. Hivyo ni vizuri chama kuwa na ukwasi sahihi.

Uwepo na matumizi ya sera hii itawezesha chama kuwa na:-

a) Kuanzisha mfumo wa kugharimia mahitaji ya ukwasi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.
b) Kuweka mfumo wa kusimamia upatikanaji wa fedha na tahadhari dhidi ya upungufu wa ukwasi;
c) Kuweka mfumo wa kupima, kutambua na kutathimini mahitaji ya ukwasi wakati wote;
d) Kuweka vigezo vya kuwasilisha matokeo ya upimaji wa mahitaji ya ukwasi;
e) Kuweka mwongozo wa kusimamia mahitaji ya ukwasi wa SACCOS
f) Kubainisha shughuli mahususi za upatikanaji wa fedha na mahitaji ya ukwasishaji;
g) Kuandaa mfumo wa dharura wa kupata fedha kukabili mahitaji ya ukwasishaji.

Kwa ujumla madhumuni makuu ya Sera hii ya Ukwasi, Mali na Dhima ni kukiwezesha chama kudhibiti na kusimamia maeneo yote yanayohusika na ujenzi wa mtaji kwa upande mmoja na vyanzo vyote vya mali iliyotengeneza mtaji kwa upande mwingine. Utambuzi wa majanga yanayoweza kuathiri ukuaji wa shughuli za kiuchumi za chama na Udhibiti wa majanga hayo ili yasiathiri matokeo ya uendeshaji wa chama kifedha.

Manufaa ya Ukwasishaji kwenye Chama ni mengi ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

i. Kusimamia na kufuatilia miamala yote ya fedha zinazoingia kwenye chama kwa kila kipindi.
ii. Kupunguza gharama za kuhifadhi fedha zisizohitajika kwenye matumizi ya wakati huo.
iii. Kuwezesha utoshelevu wa mahitaji ya chini ya hifadhi ya fedha na ukwasi mwingine unaohitajika kwa wakati.
iv. Kuepusha gharama za nyongeza zinazotokana na mikopo ya haraka na ukwasi wa kulazimishwa na Taasisi za kifedha zinazokitumia chama kama njia rahisi ya biashara ya fedha kwa njia ya mikopo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MENEJIMENTI YA UKWASI, MALI NA DHIMA KATIKA CHAMA

2.1 Watu wanaowajibika na usimamizi wa Ukwasi, Mali na Dhima za Chama

Mtu atakeyehusika na usimamizi wa ukwasi katika chama atakuwa ni Meneja wa chama kwa niaba ya Bodi ya chama na endapo hatakuwepo chamani jukumu hilo litakaimishwa kwa Mhasibu wa chama. Meneja atakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Atapaswa kuhakikisha kuwa Sera ya menejimenti ya Ukwasi, Mali na Dhima inawasilishwa na kuzingatiwa na wanachama wote.

ii. Kuhakikisha Bodi ya chama inaarifiwa kuhusu hali ya ukwasi wa chama kila mara.
iii. Atawajibika katika kudhibiti hatari za ukwasi (liquidity risks).
iv. Kuhakikisha kuwa chama kinaweka sera na taratibu rafiki ambazo zitatumika kufanya tathmini ya kiwango cha ukwasi katika kipindi fulani.
v. Kuhakikisha kuwa chama kinakuwa na mfumo wa taarifa ambao utatumika kupima, kufuatilia na kutoa taarifa ya hali ya ukwasi kwa wakati.
vi. Kuhakikisha kuwa chama kinakuwa na mpango wa dharura wa ukwasi.
vii. Kuhakikisha kuwa chama kinakuwa na mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani ambao utajumuisha kufanya tathmini ya hali ya ukwasi mara kwa mara.

## 2.2 Viwianishi vinavyotumika kupima Ukwasi, Mali na Dhima

Uchambuzi wa mahitaji ya ukwasi utafanywa na Meneja wa chama kwa kuzingatia bajeti/mahitaji ya fedha taslimu na taarifa ya mtiririko wa fedha. Viwianishi kama vile "Current ratio", "Quick ratio" na "Cash ratio" zitatumika kupima kiwango cha juu cha ukwasi Kinachohitajika. Uchambuzi wa mahitaji ya ukwasi utafanywa kwa kuzingatia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 za mwaka 2018 na kanuni zake.

i. Kufanya uchambuzi wa viwianishi kama vilivyoainishwa katika Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 za mwaka 2018 na kanuni zake.

| SN | KIWIANISHI | KIWANGO (STD) |
|---|---|---|
| 1 | Vitega uchumi vya muda mfupi + Mali – dhima ya muda mfupi / Akiba na Amana za wanachama | 15 – 20% |
| 2 | Mikopo Halisi / Jumla ya mali zote. | 70 – 80% |
| 3 | Akiba + Amana/Jumla ya mali | 70 – 80% |
| 4 | Mikopo toka nje/ Jumla ya mali zote | 25% au pungufu |
| 5 | Mali zisizozalisha/Jumla ya mali | 5% - 10% |

ii. Kufuatilia tathimini ya maoteo ya mtiririko wa fedha na kuyafanyia uhakiki wa uhalisia kila mwezi.

2.3 Njia zitakazotumika kusimamia Ukwasi, Mali na Dhima za Chama

Bodi ya chama itatumia njia zifuatazo katika kusimamia ukwasi, mali na dhima za chama;

i. Menejimenti wa ukwasi, Mali na Dhima katika chama itakuwa chini ya Bodi ya chama na kamati zake na kutoa taarifa kwenye mkutano mkuu wa wanachama juu ya mwenendo mzima wa menejimenti ya ukwasi, mali na dhima kwa maslahi mapana ya wanachama.

ii. LESA SACCOS itahakikisha kwamba wakati wote kunakuwepo na ukwasi usiopungua Tshs 20,000,000/= nje ya matengo ya mikopo mibaya kwa ajili ya mahitaji ya wanachama yatakayojitokeza wakati wowote na pia kiwango hiki kinaweza kubadilika kutokana na ukuaji wa Chama.

iii. Mwanachama yoyote wa LESA SACCOS atakopeshwa kuanzia Tshs 100,000/= hadi Tshs 100,000,000/= kwa mkopo mmoja wa maendeleo na Tsh. 100,000 hadi Tsh. 10,000,000 kwa mkopo wa dharura na Tsh. 100,000 hadi Tsh.2,000,000 kama mkopo wa chapchap kwa kuzingatia sera ya mikopo na vigezo vingine muhimu katika ukopeshaji wa fedha.

iv. LESA SACCOS itafanya udhibiti wa Ukwasi, Mali na Dhima zake kwa kutumia uwiano ulioidhinishwa na Baraza la Vyama vya Akiba na Mikopo Duniani (WOCCU) kwa lengo la kupima ufanisi wa fedha na tathmini ya uendeshaji wa chama.Management ya chama itataoa taarifa kwa Bodi ya chama kila robo mwaka juu ya mwenendo wa hali halisi ya Ukwasi, Mali na Dhima za chama kwa kuzingatia ''PEARLS Ratios" zilizotolewa na Baraza la Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo Dunia na kutoa tafsiri sahihi katika vikao vya Bodi ili iweze kufanya maamuzi stahiki wakati kwa maslai mapana ya Chama na Wanachama kwa ujumla.

v. LESA SACCOS LTD itakuwa na mali zinazobadilika kirahisi kuwa fedha taslimu (liquidity Assets) kwa uwiano usiopungua 15% ya jumla ya dhima za muda mfupi

vi. Menejimenti itafanya upembuzi wa kina mara kwa mara kuhusu usimamizi wa Ukwasi, mali na Dhima na kutoa taarifa kwa Bodi ya chama ili waweze kutoa maamuzi sahihi ya kifedha na uwekezaji katika chama.

vii. LESA SACCOS LTD itaweka malengo ya uwekezaji ambayo yataendana na mahitaji ya ukwasi wa chama.

viii. Kufuatilia tofauti ya riba ya akiba na riba ya mikopo ili kuweka kiwango cha riba kitakachokidhi mahitaji ya chama.

ix. LESA SACCOS LTD imeweka kiwango cha juu cha Tsh.300,000,000 kwenye ukomo wa kukopa kutoka taasisi nyingine za kifedha.

x. LESA SACCOS LTD imeweka utaratibu wa Kufanya tathmini ya madeni kila mwaka na kuangalia kama chama kinakidhi mahitaji ya muda mfupi.

2.4 Kiwango cha juu na chini cha fedha taslimu

Fedha taslimu na amana za muda mrefu hazitakuwa chini ya kiwango kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria na hazitakuwa zaidi ya kiwango kinachohitajika kama kitakavyowekwa na Bodi. Hivyo kiwango cha chini cha fedha taslimu kitakuwa Tsh.100,000 na kiwango cha juu kitakuwa Tsh.650,000 kama kitakavyofanyiwa mapitio kila baada ya mwaka kutegemea na ukuwaji wa chama.

2.5 Kiwango cha juu cha fedha taslimu kwenye kasiki

Chama kitakuwa na kiasi cha fedha taslimu Tsh.650,000 "Petty Cash" kwenye kasiki kwa kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya dharura. Katika kukinga majanga ya fedha taslimu, Chama kitaweka bima ya fedha ikiwa pamoja na udhibiti thabiti wa matumizi na kuhakikisha fedha husika zinatunzwa kwa usalama wa hali ya juu.

2.6 Utaratibu wa utoaji wa taarifa ya hali ya ukwasi

Menejimenti ya chama itatoa taarifa ya hali ya ukwasi kwa Bodi ya chama kila robo mwaka juu ya mwenendo wa hali halisi ya Ukwasi, Mali na Dhima za chama kwa kuzingatia uwiano (ratios) zilizowekwa kwa kuzingatia sheria na kutoa tafsiri sahihi katika vikao vya Bodi ili iweze kufanya maamuzi stahihi.

2.7 Utaratibu wa mara kwa mara wa kuchambua Ukwasi, Mali na Dhima

Chama kitafanya tathmini ya bakaa ya mwezi ya amana na madeni yake kila mwisho wa mwezi ili kuchambua mahitaji ya ukwasi wa chama.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAHITAJI YA UKWASI

Mahitaji ya ukwasi katika LESA SACCOS utazingatia masuala yafuatayo;

**i.** LESA SACCOS LTD itachambua mahitaji ya ukwasi kwa muda usiopungua mwezi mmoja kwa hatua za muda mfupi (short term measure) ili kuhakikisha ukwasi/fedha zinazotosheleza kwa muda husika kwa ajili ya kutoa huduma ya mikopo kwa wanachama.

**ii.** LESA SACCOS LTD itachambua mahitaji ya ukwasi kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili kwa hatua za muda mrefu (long-term measure) ili kuhakikisha kwamba ukwasi/fedha zinakuwepo wakati wote kwa ajili ya kukopesha wanachama.

**iii.** LESA SACCOS LTD itaweka mpango wa dharura wa kunusuru hali mbaya ya ukwasi itakayojitokeza. Katika kuweka mpango wa dharura chama kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

a) Kufanya upembuzi wa kina wa wanachama wanaotarajia kukopa na kufanya usimamizi wa karibu katika ukusanyaji wa mikopo na riba yake. Aidha chama kitatoa mikopo kwa kiwango cha kati kwa wanachama wengi Zaidi wenye

maombi ya mikopo midogo midogo, na ile mikubwa itafikiriwa baada ya kutathmini hali ya ukwasi.

b) Kuwekeza kwenye mali zinazobadilishika kwa urahisi kuwa fedha taslimu, mfano kununua Hisa kwenye makampuni yaliyosajiliwa na soko la hisa la Dar-es-salaam (DSE) na kuwekeza kwenye dhamana za serikali, Amana za Serikali zinazohamishika (treasury bills) .

c) Kuwekeza katika amana za muda mfupi kama vile amana za muda maalum (FDR) za miezi 3, miezi 6 miezi 9 au miezi 12 kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wanachama wakati wote kama sera ya uwekezaji inavyoelekeza.

iv). LESA SACCOS itapitia na kusimamia muundo wa hali halisia ya mali na dhima ili kudhibiti hatari ya riba (interest rate Risks) zinazoweza kujitokeza.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UKOPAJI KUTOKA NJE

Chama kinaweza kukopa kutoka nje (Taasisi nyingine za fedha) ili kukidhi mahitaji ya fedha kwa ajili ya kukopesha wanachama wake. Chama kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo wakati wa kukopa kutoka taasisi nyingine za fedha;

i. Endapo LESA SACCOS italazimika kukopa fedha kutoka kwenye taasisi nyingine za kifedha, itakopa kiwango kisichozidi 25% ya mali zote za chama (25% of total Assets).

ii. Kupitia Mkutano Mkuu wa Chama wa mwaka wakati wote LESA SACCOS itaweka kiwango cha juu kabisa cha fedha cha kukopwa

nje (na taasisi nyingine za kifedha au benki) kulingana na mahitaji ya wanachama. Baada ya mkutano huo kupitisha kiwango hicho na Mrajis wa Vyama vya Ushirika atajiridhisha na kuidhinisha kutoa hati ya ukomo wa madeni baada ya kufanya upembuzi wa kutosha katika maombi hayo kama inavyoelekezwa na Sheria na Kanuni.

iii. LESA SACCOS itaweka mpango madhubuti wa maandishi wa jinsi ya kupunguza kukopa mikopo nje "reduction of external borrowings plan" kwa kiwango kisichozidi 25% ya mali zote za chama ndani ya miaka mitano.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAJUKUMU YA BODI YA CHAMA

Ili chama kiweze kufikia malengo yake makuu ambayo ni kutoa huduma ya mikopo kwa wanachama wake, Bodi ya chama inapaswa kuhakikisha kuwa sera hii inatekelezwa ipasavyo. Bodi ya chama itakuwa na majukumu yafuatayo;

i. Kuipitia na kuifanyia marekebisho sera hii kulingana na mahitaji ya chama kwa kuzingatia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na kanuni zake.

ii. Kuhakikisha kuwa sera hii ya Menejimenti ya Ukwasi, Mali na Dhima inaendana na sera nyingine za chama.

iii. Kuisimamia Menejimenti ya chama katika utekelezaji wa sera hii.

## SEHEMU YA SITA

### 6.0 MPANGO WA DHARURA WA UKWASISHAJI

LESA SACCOS LTD itaandaa mpango wa dharura wa kupata fedha ili kukabili upungufu wa fedha utakaojitokeza. Mpango utazingatia mahitaji ya kisheria ya kupata hati ya ukomo wa madeni na makubaliano ya muda mrefu baina ya LESA SACCOS LTD na taasisi za fedha. Utakuwa ni wajibu wa Menejimenti kuandaa mpango huo na kuuwasilisha kwa Bodi na kuufanyia marejeo mara kwa mara kila mwaka. Aidha, chama kitatakiwa kuwasilisha mpango wa dharura wa ukwasishaji Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

6.1 Malengo ya mpango wa dharura wa ukwasishaji

i. Lengo kubwa la mpango wa dharura wa ukwasishaji ni kulinda fedha za wanachama na wadai mbalimbali na kukiwezesha chama kutoa huduma kwa wanachama wake bila kutetereka.

ii. Kuweka mwongozo ambao utaainisha na kusimamia njia bora za kuimarisha ukwasi wa chama pindi chama kitakapokabiliwa na changamoto za ukwasi.

iii. LESA SACCOS LTD itahifadhi (retain) angalau asilimia kumi na tano (15%) kama fedha kichele kutoka kwenye Akiba na Hisa za Hiari za Wanachama kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya Ukwasi ya haraka katika utoaji wa Mikopo.

iv. Kiwango cha mawekezo ya fedha za Akiba na Amana za Wanachama katika Taasisi moja ya kifedha hakitazidi asilimia ishirini na tano (25%) ya Mtaji tete wa Chama kwa tarehe ya Mizania.

Meneja wa chama atakuwa na jukumu la kuandaa mpango wa dharura wa ukwasishaji na kuuwasilisha kwa Bodi ya chama.

## SEHEMU YA SABA

### 7.0 Uidhinishwaji wa Sera

Sera hii imetayarishwa na kupitishwa na Bodi ya LESA SACCOS LTD kwa niaba ya wanachama kwa kibali cha Mrajis katika kikao chake kilichofanyika tarehe 17 Julai 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

..........................
**Mwenyekiti**

..........................
**Meneja**

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD
23 NOV 2020
KINONDONI
DAR-ES SALAAM

TANZANIA
Approved this 20TH
day of JANUARY 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies